KENYA PRIMARY SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT

KC 02

GREDI YA SITA - 2026

KISWAHILI

6

Jina:.....

Shule. .....

Gredi: ..... Tarehe:.....

Soma mazungumzo kati ya Amina na Jumakisha jibu maswali. (Alama 5).

Amina : Shikamoo Juma?

Juma : Marahaba Amina.

Amina : Umeenda wapi?

Juma : Nilitoka sokoni. Nilinunua mboga na matunda.

Amina : Vizuri. Je ulikutana na mama yetu?

Juma : Ndiyo nilimwona. Alikuwa anauza mahindi.

1. Juma ni _____ wa Amina.
   (A) mkubwa wake
   (B) kitindamimba
   (C) mdogo wake
   (D) kifungua mimba

2. Juma alikuwa anatoka wapi?
   (A) Nyumbani
   (B) Sokoni
   (C) Mtuni
   (D) Shuleni

3. Mama alikuwa anauza nini?
   (A) Mboga
   (B) Matunda
   (C) mahindi
   (D) Maembe

4. Jibu la Shikamoo ni _____
   (A) Nzuri
   (B) Marahaba
   (C) Sema
   (D) Salama

5. Juma alinunua nini
   (A) mahindi
   (B) mboga
   (C) sukari
   (D) Nyama

Soma kifungu hiki ujibu maswali. (6-10)

Mwanadamu sharti awe na mpango maishani. Asiwe mtu wa kupiga domo tu bila kutekeleza kile anachosema. Mungwana ni vitendo. Hivyo ndivyo wasemavyo waliostaarabika. Thamani ya mtu ipo kwenye yale anayotekeleza. Inasikitisha kumwona kiongozi aliyeheshimika akiwahadaa wananchi kuhusu mipango aliyo nayo kwa raia na anayokusudia kutekeleza. Wengine hudai kuwa kufikia wakati fulani watatenda hili lakini hukosa kutimiza ahadi zao kwa raia. Hivyo ni aibu kubwa na hufanya raia kupoteza imani yao kwa kiongozi wa aina hiyo.

Mwanafunzi anayelenga uongozi wa aina hii huharibu maisha yake. Hukosa hata kufanya kazi za walimu na badala yake huanza kutoa visababu na visingizio chungu nzima kuwa vijisababu na visingizio naona.

CamScanner